GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXX Nam. 6903 **12 Mei, 2021** **Bei, Shs. 6,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma na Mambo mengine yanayohusiana na hayo 229

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma na Mambo mengine yanayohusiana na hayo

TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanzia tarehe 5 Mei, 2021 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
14 Aprili, 2021

(Mhandisi Zena Ahmed Said)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA
wa

SHERIA YA KUANZISHA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA NA USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma, 2021 na itaanza kutumika baada ya kuwekwa saini na Rais.

Matumizi.

2. Sheria hii itatumika kwa:

(a) Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(b) Taasisi za Umma kwa upande wa usimamizi wa mali; na

(c) Taasisi yoyote ya Umma iliyotajwa na Waziri.

Ufafanuzi.

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"Afisa Masuuli" ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma;

"Mali" maana yake ni rasilimali yoyote inayosimamiwa na Taasisi ya Umma kutokana na tukio lililopita na faida za kiuchumi au huduma muhimu inayotarajiwa kupatikana kwa Taasisi ya Umma;

"Usimamizi wa mali" maana yake mjumuisho wa fedha, uchumi, utaalamu, usimamizi wa kiufundi na mambo mengine yoyote yanayotumika katika usimamizi wa mali kwa ajili ya kutoa huduma za kiwango kinachohitajika au bidhaa kwa gharama inayostahiki;

"Daftari la mali" maana yake ni kumbukumbu za taarifa kwa kila mali ambayo inawezesha usimamizi bora wa kifedha na kiufundi wa mali;

"Bodi" kuhusiana na Taasisi za Uwekezaji za Umma, maana yake ni Bodi za Wakurugenzi au chombo chochote cha usimamizi kwa jina lolote litakaloitwa, linalichukua nafasi zinazolingana na Bodi za Wakurugenzi;

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar, 1984;

"Afisa Mtendaji Mkuu" maana yake ni mkuu wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma iliyoanzishwa na amri ya Rais au Sheria nyengine yoyote, ambaye anahusika na uendeshaji wa shughuli za kila siku za Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

"Kampuni" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa chini ya masharti ya Sheria ya Kampuni;

"Gawio" maana yake ni kiwango cha fedha kikawaida hulipwa na Taasisi za Uwekezaji za Umma kwa wanahisa kutokana na faida;

"Mjumbe anayeingia kwa nafasi yake" maana yake ni mtu anayeteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kwa mujibu wa nafasi yake;

"Sheria inayoanzisha" kuhusiana na Taasisi ya Uwekezaji ya Umma, maana yake Sheria yoyote ambayo Taasisi ya Uwekezaji wa Umma imeanzishwa;

"Mpango wa fedha" maana yake ni bajeti na mipango mingine ya fedha inajumuisha mkopo, mipango ya uwekezaji na shughuli nyingine zilizoelezwa za Taasisi za Uwekezaji za Umma;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Sera ya Uwekezaji ya Serikali" maana yake ni waraka wowote wa Serikali unaoainisha vipaumbele, maeneo ya kimkakati, malengo na shabaha ya uwekezaji, na ambao unakidhi faida za kiuchumi zilizokusudiwa na malengo ya kifedha;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na fedha;

"Ofisi" maana yake ni Ofisi ya Msajili wa Hazina kama ilivyoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Mali ya umma" maana yake ni rasilimali yoyote inayosimamiwa na Serikali ambayo Serikali inatarajia kupata faida za kiuchumi au matumizi ya utoaji wa huduma kwa jamii kwa ujumla;

"Taasisi ya Uwekezaji ya Umma" maana yake ni Taasisi yoyote ya kibiashara, kampuni au Shirika linalomilikiwa na Serikali;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Taasisi ya Umma" ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma;

"Uwekezaji wa Umma" maana yake mali za Serikali zinazoonekana au zisizoonekana na zinajumuisha hisa, hatifungani, dhamana katika Taasisi inayojitegemea zinazotolewa na au kwa niaba ya Serikali;

"Mkataba wa utendaji" maana yake ni makubaliano ambayo yanaweka malengo kwa ajili ya kupima utendaji;

"Waziri anayehusika" kuhusiana na Taasisi ya Uwekezaji ya Umma:

(a) ambayo sio kampuni inayomilikiwa na Serikali, maana yake ni Waziri anayehusika na usimamizi wa sheria inayosimamia uanzishaji na kazi za Taasisi ya Uwekezaji ya Umma; na

(b) ambayo ni kampuni inayomilikiwa na Serikali maana yake ni Waziri mwenye hisa na mwenye kutekeleza haki zilizoambatanishwa kwenye hisa au haki nyingine zozote katika kampuni kwa niaba ya Serikali;

"Baraza la Mapinduzi" maana yake ni Baraza la Mapinduzi kama lilivyotafsiriwa katika kifungu cha 43 cha Katiba;

"Kampuni inayomilikiwa na Serikali" maana yake ni kampuni iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Kampuni ambayo Serikali ni mmliki pekee au na hisa nyingi;

"Taasisi Tanzu" maana yake ni kampuni inayomilikiwa au inayosimamiwa na kampuni nyengine; na

"Msajili wa Hazina" maana yake ni Msajili wa Hazina aliyeteuliwa chini ya masharti ya Sheria hii.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA KWA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

Kuanzish-wa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina.

4. Kunaanzishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina chini ya Wizara inayohusika na fedha.

Muhuri na nembo ya Ofisi ya Msajili wa Hazina.

5.-(1). Kutakuwa na muhuri na nembo katika umbo na namna itakavyoamuliwa na Ofisi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Ofisi katika waraka wowote yatathibitishwa na saini ya Msajili wa Hazina au Afisa mwingine yeyote wa Ofisi aliyeidhinishwa na Msajili wa Hazina.

Kazi za Ofisi.

6. Ofisi itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia uwekezaji wa umma kwa niaba ya Serikali;

(b) kuidhinisha mapendekezo ya uwekezaji ya Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(c) kusimamia na kutathmini utendaji wa jumla wa Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(d) kukuza maadili ya utawala bora katika miamala yote ya biashara, ikijumuisha utoaji wa miongozo kwa Taasisi za Uwekezaji za Umma kwenye mambo yanayohusiana na bajeti, mipango mkakati, mipango ya kibiashara, mipango ya uwekezaji na mambo mengine yoyote yanayohusiana na hayo katika kutekeleza sera za Serikali kwenye Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(e) kusimamia, kufuatilia na kutekeleza taratibu za kuundwa upya kwa Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(f) kutoa mapendekezo kwa Waziri kuhusiana na sera ya gawio;

(g) kutoa miongozo, taratibu na miongozo ya uendeshaji kwa ajili ya usimamizi wa Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(h) kuingia katika mikataba ya utendaji na Wenyeviti, au watendaji waandamizi wa Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(i) kupitia mapendekezo ya miundo ya taasisi na mishahara, miundo ya utumishi na motisha za Taasisi za Uwekezaji za Umma kabla ya kuwasilishwa kwenye Kamisheni ya Utumishi wa Umma;

(j) kupitia na kutoa mapendekezo kuhusu sera maalum na sheria zinazohusiana na uendelezaji wa Taasisi za Uwekezaji za Umma.

Uwezo wa Ofisi.

7. Ofisi itakuwa na uwezo ufuatao:

(a) kuchunguza au kutaka kujua kuhusu uendeshaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(b) kukagua na kuangalia vitabu vya hesabu, kumbukumbu, marejesho na nyaraka nyengine zozote za Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(c) kutaka taarifa yoyote, waraka na ripoti za kazi za Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(d) kumuita Mwenyekiti, mjumbe binafsi wa Bodi, Afisa Mtendaji Mkuu au watendaji waandamizi wengine wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(e) kuitisha vitabu vya hesabu, mipango na nyaraka nyengine zozote za Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(f) kutoa maelekezo juu ya usimamizi bora wa kazi katika Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(g) kufungua au kusababisha kufunguliwa kwa vyumba maalum vya uhifadhi, tajuri au vyombo vingine vyovyote vya uhifadhi ambapo inashukiwa kwamba, kutokana na sababu za msingi, kuna vitabu, kumbukumbu, hesabu au nyaraka nyengine zozote za Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(h) kutaka na kuchukua baadhi ya nyaraka kwa njia ya nakala laini au nakala ngumu za vitabu vyovyote, kumbukumbu, hesabu au nyaraka;

(i) kumtaka Afisa Mtendaji Mkuu yeyote au Afisa Mwandamizi wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kuwasilisha taarifa kama zitakavyohitajika;

(j) kufanya au kuwezesha kufanyika kwa ukaguzi maalum kwa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma; na

(k) kufanya jambo jengine lolote kama itakavyojitokeza au kuwezesha utekelezaji wa kazi za Ofisi chini ya Sheria hii.

Uteuzi wa Msajili wa Hazina.

8.-(1) Kutakuwa na Msajili wa Hazina ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Msajili wa Hazina atakuwa ni Mkuu wa Ofisi na atasimamia kazi za kila siku.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Msajili wa Hazina ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza au inayofanana na katika fani ya uchumi, biashara, fedha, sheria, utawala wa umma au fani nyengine yoyote inayohusiana na hizo kutoka katika taasisi ya elimu inayotambulika; na

(c) mwenye uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba katika utumishi wa umma.

Kazi za Msajili wa Hazina.

9. Msajili wa Hazina atakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuamua uteuzi wa watendeji wa Ofisi na kuwapangia majukumu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma;

(b) kuidhinisha mgao wa faida ya mwaka na kutangaza mgao, ziada au mchango wa Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(c) kuainisha Taasisi za Uwekezaji za Umma katika madaraja mbalimbali;

(d) kusajili na kulihifadhi daftari la Taasisi za Uwekezaji za Umma ikijumuisha taarifa zifuatazo:

(i) jina la Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(ii) hati ya uanzishaji;

(iii) mwaka wa kuanzishwa;

(iv) lengo la Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(v) aina ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(vi) makao makuu ya Ofisi na anuani ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(vii) jina la Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(viii) mtaji wa uanzishaji wa Taasisi ya Uwekezaji wa Umma;

(ix) jina la Wizara inayohusika na Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(x) jina la Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(e) kuwa mmiliki pekee wa uwekezaji wa Umma na mhifadhi wa mali zote za Umma kwa niaba ya Serikali;

(f) kufanya tathmini ya mradi mpya unaowasilishwa na Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kwa madhumuni ya upatikanaji wa fedha;

(g) kuishauri Serikali juu ya mambo yanayohusiana na Taasisi za Uwekezaji za Umma na usimamizi wa mali za umma;

(h) kuanzisha misingi ya usimamizi na uzoefu wa uendeshaji kwa Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(i) kuainisha vigezo vya utendaji, vipimo na tathmini kwa wajumbe wa Bodi za Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(j) kutoa miongozo kwa Taasisi za Uwekezaji za Umma katika mikataba ya utendaji;

(k) kuidhinisha sera za utendaji wa Taasisi za Uwekezaji za Umma kabla ya kusainiwa na Waziri anayehusika;

(l) kuchambua na kutoa mapendekezo kuhusiana na mipango mkakati na mipango ya mwaka ya Taasisi za Uwekezaji za Umma kabla ya kuidhinishwa;

(m) kufuatilia kwa karibu na kusimamia mambo ya fedha ya Taasisi za Uwekezaji za Umma na kuweka taratibu za:

(i) kupunguza matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija kwa Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(ii) kuzuia upotevu wa fedha unaotokana na uzembe, ukosefu wa hadhari, wizi, ukosefu wa uaminifu au vyenginevyo;

(iii) kuongeza kiwango cha gawio kitakacholipwa au kuhaulishwa kutokana na mapato kwa Msajili wa Hazina;

(n) kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mwenendo wa biashara wa Taasisi za Uwekezaji za Umma;

(o) kumshauri Waziri anayehusika juu ya namna ya kuisaidia Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kutokana na vikwazo na hatua zinazopaswa kuchukuliwa;

(p) kusimamia biashara za Taasisi za Uwekezaji za Umma kwa:

(i) kupitia mambo ya fedha na utendaji wa Taasisi za Uwekezaji za Umma na kushauri hatua kama vile kuundaji upya au kuimarisha utendaji wake;

(ii) kumshauri Waziri anayehusika kuhusiana na uundaji upya wa Taasisi yoyote ya Uwekezaji wa Umma;

(iii) kufanya tathmini ya utendaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma na kutoa mapendekezo kwa Waziri anayehusika;

(iv) kufanya ukaguzi maalum kwa mapato na matumizi ya Taasisi yoyote ya Uwekezaji wa Umma

(q) kutekeleza kazi nyengine zozote kama itakavyoagizwa na Waziri.

Uwezo wa kukasimu kazi.

10.-(1) Msajili wa Hazina anaweza, kwa hati ya maandishi, kukasimu kazi yoyote miongoni mwa kazi zake kwa mtendaji yeyote wa Ofisi;

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hati ya kukasimu itaeleza masharti, taratibu na miongozo mingine yoyote ya Msajili wa Hazina.

(3) Kazi zilizokasimiwa chini ya kifungu hiki, zitachukuliwa kuwa zimetekelezwa na Msajili wa Hazina.

Watendaji wa Ofisi.

11.-(1) Kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma, Ofisi itaajiri watendaji kwa mujibu wa muundo wa taasisi wa Ofisi.

(2) Kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii, Ofisi inaweza kuanzisha Idara, Sehemu au Vitengo vitakavyoongozwa na wakuu au watendaji wengine kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Katazo kwa Msajili was Hazina na Watendaji.

12. Msajili wa Hazina au mtendaji yeyote aliyeajiriwa na Ofisi hatateuliwa kuwa Mwenyekiti au mjumbe wa Bodi ya Taasisi yoyote ya Uwekezaji ya Umma.

SEHUMU YA TATU
KUANZISHWA KWA TAASISI ZA UWEKEZAJI ZA UMMA

Kuanzishwa kwa Taasisi za Uwekezaji za Umma.

13. Taasisi yoyote ya Uwekezaji ya Umma itaanzishwa ama kwa:

(a) amri iliyotolewa na Rais iliyotangazwa katika Gazeti;

(b) Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi; au

(c) Sheria ya Kampuni.

Taratibu za kuanzisha Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

14.-(1) Kabla ya kuanzisha Taasisi yoyote ya Uwekezaji ya Umma chini ya sharti lolote miongoni ya masharti ya kifungu cha 13 cha Sheria hii, Taasisi ya Umma itawasilisha kwa Msajili wa Hazina nyaraka zifuatazo:

(a) upembuzi yakinifu;

(b) mpango wa biashara; na

(c) taarifa nyengine yoyote inayohusiana na uanzishaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

(2) Msajili wa Hazina, baada ya kupokea na kupitia pendekezo la mradi, atawasilisha mapendekezo kwa Baraza la Mapinduzi kwa mazingatio.

Uwasilishaji wa mapende-kezo ya mradi.

15. Kabla ya kuwasilisha kwenye mamlaka yoyote husika kwa ajili ya idhini, pendekezo lolote linalohusiana na mradi wa Taasisi ya Uwekezaji

ya Umma au kati ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma na kampuni binafsi au mwekezaji binafsi litawasilishwa kwa Msajili wa Hazina kwa ajili ya kutoa mapendekezo.

Hadhi ya kisheria ya Taasisi ya Uwekezaji wa Umma.

16. Taasisi ya Uwekezaji ya Umma inayoanzishwa chini ya Sheria hii itakuwa:

(a) chombo chenye kujitegemea, endelevu, chenye muhuri na kwa jina lake, kitakuwa na uwezo wa:

(i) kupata, kumiliki na kuondosha mali kwa ajili ya utekelezaji wa madhumuni ya Taasisi ya Uwekezaji wa Umma;

(ii) kushitaki au kushitakiwa;

(iii) kuingia katika mkataba wowote au muamala mwingine wowote kwa ajili ya utekelezaji wa kazi au utekelezaji wa uwezo wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(iv) kukopa, kukopesha au kupokea msaada wa kiwango chochote cha fedha kutoka taasisi yoyote ya fedha kwa madhumuni ya utekelezaji wa kazi za Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma.

Uteuzi wa Afisa Mtendaji Mkuu.

17.-(1) Taasisi ya Uwezekaji ya Umma itakuwa na Afisa Mtendaji Mkuu anayeteuliwa na Rais.

(2) Afisa Mtendaji Mkuu atakuwa Mkuu wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma na atahusika na kazi za kila siku.

(3) Afisa Mtendaji Mkuu atawajibika kwa Bodi na atatoa taarifa za utendaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma katika kila mkutano wa Bodi.

Ajira ya watendaji.

18.-(1) Kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma, Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itaajiri watendaji na watendaji waandamizi kama watakavyohitajika katika utekelezaji wa kazi za Taasisi ya Uwezekaji ya Umma.

(2) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, endapo Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itateua wakuu wa Idara, Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itamtaarifu Waziri anayehusika ikiainisha:

(a) jina, anuani na taarifa nyengine binafsi za mteule;

(b) sifa za mteule; na

(c) vigezo vilivyotumika kumteua mteule.

(3) Afisa Mtendaji Mkuu atawasilisha nakala ya taarifa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki kwa Msajili wa Hazina ikijumuisha nakala ya barua ya uteuzi.

(4) Upandishaji wa vyeo na hatua za kinidhamu zinazohusiana na watendaji waandamizi wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma zitakuwa ndani

ya mamlaka ya Bodi na zitatekelezwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi w Umma.

(5) Isipokuwa kwa uteuzi wa Rais, hakuna muajiriwa au afisa wa Taasisi yoyote ya Umma au Taasisi ya Uwekezaji ya Umma atakayehamishwa kwenda Taasisi ya Uwekezaji ya Umma bila ya idhini ya Bodi.

(6) Bodi itakuwa na uwezo wa kumuajiri, kumsimamisha au kumfuta mtendaji yeyote au mtendaji mwandamizi wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Masharti ya utumishi kwa watendaji.

19.-(1) Bodi itaweka masharti ya utumishi kwa watendaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma ambayo:

(a) yatakuwa yanaendana masharti ya mikataba ya utendaji ya watendaji; na

(b) yataweka bayana maslahi ambayo watendaji wanastahiki;

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, masharti ya utumishi yaliyowekwa kwa Afisa Mtendaji Mkuu na wakuu wa Idara:

(a) yatakuwa yenye haki na usawa;

(b) yatazingatia sifa na uzoefu;

(c) yataendana na kazi ambazo zinatarajiwa kutekelezwa; na

(d) yatakuwa yanaenda sambamba na masharti ya utumishi ya Taasisi nyengine za Uwekezaji za Umma.

Muundo wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

20.-(1) Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itakuwa na muundo kama itakavyoamuliwa na Bodi na kuidhinishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Bodi itaanzisha Idara, Sehemu au Vitengo na kuteua watendaji waandamizi kuwa wakuu wa Idara, Sehemu au Vitengo kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii.

Bodi ya Wakurugenzi.

21.-(1) Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ambayo itauundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais; na

(b) Wajumbe wengine wasiopungua wanne na wasiyozidi sita ambao watateuliwa na Waziri anaehusika ikujumuisha wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao.

(2) Kabla ya uteuzi wa wajumbe wa Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma walioainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1)(b) cha kifungu hiki, mamlaka ya uteuzi itawasilisha orodha ya majina katika Ofisi, isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, kwa ajili ya kutathimini sifa zao na uzoefu.

(3) Ofisi itaweka taratibu za kuwasilisha orodha ya majina.

(4) Baada ya mtu kuteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi, Ofisi itawezesha kutolewa tangazo litakalochapishwa katika Gazeti litakaloainisha jina la mtu na Bodi ambayo ameteuliwa.

(5) Bila kuathiri ujumla wa masharti ya Sheria hii, watu wafuatao hawatasitahiki kuteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi:

(a) Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi;

(b) Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(c) Mkaguzi Mkuu wa Ndani na Watendaji wa Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani;

(d) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na

(e) Msajili wa Hazina na watendaji wa Ofisi.

(6) Bodi itawajibika kwa Waziri anayehusika katika utaratibu uliowekwa katika Sheria hii.

Katibu wa Bodi.

22. Bodi itamteua Katibu kutoka miongoni mwa maafisa waandamizi wa umma wenye sifa katika Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Muda wa Bodi.

23.-(1) Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nyadhifa zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja tu.

(2) Mjumbe wa Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma anaweza kuondolewa ikiwa mjumbe huyo:

(a) amekutwa na hatia kwa kosa la kwenda kinyume na nafasi ya ujumbe;

(b) amepoteza sifa za kuteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi;

(c) akiwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, amesita kuwa na nafasi hiyo;

(d) ameshindwa kufuata masharti ya Utumishi wa Umma au masharti ya mkataba wa utendaji;

(e) ama peke yake au kwa pamoja na wajumbe wengine wa Bodi, ameshindwa kufikia malengo ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma yaliyowekwa katika mpango mkakati;

(f) ameshindwa kuhudhuria bila ya sababu au ruhusa ya Mwenyekiti kwa vikao vitatu au zaidi mfululizo vya Bodi;

(g) ameshindwa kutekeleza kazi kutokana na ugonjwa wa mwili au akili; au

(h) ametiwa hatiani kwa kosa linalohusika na uaminifu, udanganyifu au kukosa maadili.

(3) Afisa Mtendaji Mkuu, ndani ya siku saba baada ya kuondolewa kuwa mjumbe yeyote wa Bodi, ataijulisha Ofisi juu ya kuondolewa kwa mjumbe kwenye Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Ukomo wa kuwa Mjumbe.

24. Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, mtu yeyote hatachaguliwa kuwa mjumbe wa Bodi za Wakurugenzi zaidi ya tatu kwa wakati mmoja.

Kuvunjwa kwa Bodi.

25. Kwa maslahi ya umma, Waziri anayehusika kwa kushauriana na Rais anaweza, wakati wowote, kuvunja Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kwa tangazo la kisheria lililochapishwa katika Gazeti la Serikali.

Majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi.

26.-(1) Kwa ufanisi na utendaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma, Bodi ya Wakurugenzi itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) itatunga, itasimamia na itafuatilia sera ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(b) itaidhinisha bajeti, kanuni za fedha, mpango kazi na sera nyengine za ndani ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(c) itatoa miongozo kwa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(d) itasimamia maadili, uweledi na hadhi ya watendaji ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(e) itahakikisha kwamba Taasisi ya Uwekezaji ya Umma inafuata mpango mkakati, mpango wa kupunguza athari na hatua zinazolenga kukuza utendaji;

(f) iwe na uangalifu katika kudhibiti vihatarishi na kusimamia mali;

(g) itaendana na Sheria zilizopo, kanuni, kanuni za maadili na viwango vya utendaji vinavyokubalika;

(h) itakeleza kwa maslahi mapana ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma na Serikali;

(i) itatunga na itatekeleza taratibu za kulinda biashara wakati Taasisi ya Uwekezaji ya Umma ipo katika hali mbaya kifedha;

(j) itahakikisha kwamba Taasisi ya Uwekezaji ya Umma ina mikakati ya kifedha na rasilimali watu inayohitajika kwa ajili ya kufikia malengo yake;

(k) itasimamia matumizi ya miradi ya maendeleo;

(l) itasimamia uchukuaji na utoaji wa mitaji;

(m) itasimamia na itapitia usimamizi wa utendaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma; na

(n) itaidhinisha kanuni za maadili na kanuni za fedha, itaongeza ari na uweledi kwa waajiriwa, uongozi na wajumbe wa Bodi.

(2) Bodi ya Wakurugenzi itawajibika kwa mamlaka ya uteuzi.

Kamati za Bodi.

27.-(1) Bodi itaanzisha Kamati ya Ukaguzi na Kamati nyengine zozote kama itakavyoamua.

(2) Wajumbe wa Kamati watakuwa miongoni mwa wajumbe wa Bodi.

(3) Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kuisaidia Kamati za Bodi kutekeleza kazi zake.

Mikutano ya Bodi.

28.-(1) Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itakutana kikawaida mara moja kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana wakati mwengine wowote pale inapohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

(2) Taratibu za mikutano ya Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma zitaelezwa katika Sheria ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma husika au Amri.

Kueleza maslahi ya mjumbe.

29.-(1) Mjumbe yeyote wa Bodi, kwa namna yoyote ile anayo ama maslahi ya kifedha au maslahi mengine yoyote, ataeleza kwa Bodi aina ya maslahi yake mwanzo wa mkutano.

(2) Mjumbe ambaye ameeleza maslahi yake chini ya kifungu kidogo cha (1) hatotakiwa:

(a) kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya Bodi yanayohusiana na jambo hilo; na

(b) kuhusika katika maamuzi yoyote ya Bodi kuhusiana na jambo hilo.

Maslahi ya Bodi.

30. Msajili wa Hazina, kwa kushauriana na mamlaka husika, ataamua posho, ada na maslahi mengine kulipwa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Mkutano Mkuu wa Mwaka.

31.-(1) Mkutano wa Mwaka utaitishwa kwa kuzingatia aina ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kuweka miongozo ya kuitisha Mkutano ya Mwaka.

SEHEMU YA NNE
UWAJIBIKAJI WA TAASISI ZA UWEKEZAJI ZA UMMA

Mpango Mkakati.

32. Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itaandaa mpango mkakati kwa mujibu wa miongozo itakayotolewa na Msajili wa Hazina kila baada ya muda.

Mkataba wa Utendaji wa Afisa Mtendaji Mkuu.

33.-(1) Baada ya uteuzi, Afisa Mtendaji Mkuu atatakiwa kuingia katika mkataba wa utendaji kati yake na Bodi kwa mujibu wa vigezo na masharti yaliyoainishwa na Msajili wa Hazina.

(2) Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itamuelekeza Afisa Mtendaji Mkuu kuwasilisha nakala ya mkataba wa utendaji ulioingiwa kati ya Bodi na Afisa Mtendaji Mkuu kwa:

(a) Waziri anayehusika;

(b) Msajili wa Hazina; na

(c) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Tathmini ya mkataba wa utendaji.

34.-(1) Mwenyekiti atafanya tathmini ya mkataba wa utendaji kila mwaka baina ya Bodi na Afisa Mtendaji Mkuu na atatayarisha ripoti ya tathmini.

(2) Ripoti ya tathmini iliyoanishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki itawasilishwa kwa Msajili wa Hazina.

(3) Endapo Afisa Mtendaji Mkuu atashindwa kutekeleza kwa mujibu wa vigezo na masharti yaliyowekwa ndani ya mkataba wa utekelezaji, Mwenyekiti wa Bodi atawasilisha taarifa pamoja na maelezo ya kutosha kwa Waziri anayehusika na kwa Msajili wa Hazina kuhusiana na kushindwa kutekeleza kwa Afisa Mtendaji Mkuu huyo.

Mikataba ya Utendaji kwa wajumbe wa Bodi.

35.-(1) Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma wataingia katika mikataba ya utekelezaji kati yao na Msajili wa Hazina kwa mujibu wa vigezo na masharti yaliyoainishwa na Ofisi.

(2) Msajili wa Hazina atafanya tathmini ya mikataba ya utendaji ya Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma na kuwasilisha kwa Waziri anayehusika kwa mazingatio.

Utayarishaji wa mpango wa fedha.

36.-(1) Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itaandaa mpango wa fedha wa kila mwaka.

(2) Mpango wa fedha ulioandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki utafuata masharti kama yalivyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(3) Mpango wa fedha chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utawasilishwa kwa Ofisi ndani ya siku tisini kabla ya kuanza mwaka mwingine wa fedha kwa kuidhinishwa.

(4) Taasisi ya Uwekezaji ya Umma haitokwenda kinyume na mpango wa fedha ulioidhinishwa na Ofisi.

(5) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, Taasisi ya Uwekezaji ya Umma inaweza kupitia mpango wa fedha pale inapohitajika na itawasilisha katika Ofisi kwa kuidhinishwa.

(6) Taasisi ya Uwekezaji ya Umma yoyote ambayo itashindwa kufuata masharti ya kifungu hiki, itatakiwa kumtaarifu Msajili wa Hazina sababu za kushindwa huko.

Uwezo wa kukopa.

37.-(1) Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itakuwa na uwezo wa kukopa kwa mujibu wa vigezo na masharti yaliyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(2) Endapo Taasisi ya Uwekezaji ya Umma inakusudia kukopa, kabla haijawasilisha maombi ya mkopo kwa mamlaka husika, itaonyesha mipango ya kukopa na mikakati ya ulipaji mkopo katika mpango wa fedha.

Uwezo wa kuwekeza.

38.-(1) Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itakuwa na uwezo wa kuwekeza kwa mujibu wa Sera ya Uwekezaji ya Serikali.

(2) Uwekezaji wowote wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma utamilikiwa na Msajili wa Hazina kwa niaba ya Serikali.

(3) Baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, Taasisi ya Uwekezaji ya Umma ambayo ina uwekezaji wowote itawasilisha kwa Msajili wa Hazina kwa madhumuni ya usajili pamoja na taarifa zifuatazo:

(a) jina la uwekezaji;

(b) malengo ya uwekezaji;

(c) mtaji wa uwekezaji;

(d) mtu au mamlaka inayoendesha uwekezaji kwa niaba ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma; na

(e) taarifa nyengine zozote zinazohusiana na uwekezaji huo.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, Msajili wa Hazina atakuwa na uwezo wa kutoa miongozo yoyote pale ikihitajika kwa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Utayarishaji wa taarifa za fedha.

39. Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itatayarisha na itawasilisha katika Ofisi taarifa za fedha zilizokaguliwa kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Matawi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

40.-(1) Baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, Taasisi yoyote ya Uwekezaji ya Umma ambayo ina Tawi lolote itatakiwa kumtaarifu Msajili wa Hazina.

(2) Msajili wa Hazina anaweza kutoa masharti kuhusiana na Tawi lolote la Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kwa madhumuni ya kupata ufanisi na usimamizi bora.

(3) Masharti chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki yanaweza kutolewa ama kwa Bodi au kwa Afisa Mtendaji Mkuu na yanaweza kujumuisha:

(a) muundo wa Bodi na taratibu za uteuzi wa Tawi la Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(b) mikataba ya utendaji baina ya wajumbe wa Bodi wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma na watendaji waandamizi na Tawi la Taasisi ya Uwekezaji ya Umma; na

(c) jambo jengine lolote linalohusiana na Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Katiba ya Tawi ambayo inakwenda kinyume na Sheria hii itatakiwa kurekebishwa ili iendane na masharti ya Sheria hii.

Kuwasilisha malipo kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

41.-(1) Ofisi itaitaka Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kuwasilisha malipo kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa kiwango ambacho kitakachoamualiwa na Waziri kama ifuatavyo:

(a) kwa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma inayozalisha faida, gawio litalipwa; na

(b) kwa Taasisi nyengine ya Uwekezaji ya Umma isiyozalisha faida, uwiano wa mapato utalipwa.

Fedha na rasilimali za Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

42. Taasisi ya Uwekezaji ya Umma itakuwa na fedha na rasilimali ambazo zinatokana na:

(a) mtaji uliolipwa;

(b) fedha nyengine zilizotolewa na Serikali kwa njia ya mkopo, mtaji au msaada kwa ajili ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(c) fedha nyengine yoyote iliyokopwa na Taasisi ya Uwekezaji ya Umma; au

(d) fedha yoyote ambayo kwa namna yoyote italipwa kwa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kutokana na utekelezaji wa kazi zake.

SEHEMU YA TANO
KUWASILISHA TAARIFA KATIKA OFISI

Wajibu wa kuwasilisha taarifa.

43.-(1) Ofisi inaweza kumuagiza Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kuwasilisha taarifa yoyote au waraka wowote ndani ya muda uliyoainishwa.

(2) Afisa Mtendaji Mkuu atafuata maelekezo ndani ya kipindi kama kilivyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Utaratibu wa kuwasilisha taarifa.

44. Ofisi itaweka utaratibu wa kuwasilisha taarifa zinazohusiana na utekelezaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kwa Waziri, Waziri anayehusika na Msajili wa Hazina.

SEHEMU YA SITA
UKAGUZI NA UCHUNGUZI

Ukaguzi.

45.-(1) Ofisi inaweza, kwa taarifa ya maandishi, kufanya ukaguzi kwa Taasisi yoyote ya Uwekezaji ya Umma.

(2) Ukaguzi chini ya Sheria hii unaweza kuhusisha jambo lolote linalohusiana na utendaji, kazi, biashara, miamala, mali, madeni au mambo mengine yoyote ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Uteuzi wa wakaguzi.

46. Ofisi inaweza kuteua miongoni mwa watendaji wake kuwa wakaguzi kwa vigezo na masharti yalioanishwa katika hati ya uteuzi.

Uwezo wa kukagua.

47. Mkagauzi atakuwa na uwezo wa:

(a) kuingia katika majengo na kupata taarifa yoyote ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma; na

(b) kumtaka Afisa Mtendaji Mkuu au mtendaji yeyote wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kutoa taarifa yoyote au nyaraka.

Uchunguzi.

48.-(1) Endapo uchunguzi unahitajika, Ofisi, baada ya kushauriana na Waziri anayehusika, itamtaka mtu yeyote au mamlaka yoyote kufanya uchunguzi kwa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

(2) Uchunguzi chini ya kifungu hiki unaweza kuhusisha utendaji, kazi, biashara, miamala, mali, madeni au mambo mengine yoyote ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Uwezo wa mchunguzi.

49.-(1) Mchunguzi atakuwa na uwezo wa:

(a) kumuita Afisa Mtendaji Mkuu, Mwenyekiti, mjumbe wa Bodi au mwajiriwa yeyote wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma;

(b) kumuita Afisa Mtendaji Mkuu, Mwenyekiti, mjumbe wa Bodi au mwajiriwa yeyote wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kutoa nyaraka zozote ambazo zipo chini ya hifadhi au mamlaka yake;

(c) kumtaka Afisa Mtendaji Mkuu, Mwenyekiti, mjumbe wa Bodi au mwajiriwa yeyote wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kutoa msaada unaostahiki kuhusiana na uchunguzi; na

(d) kumtaka Afisa Mtendaji Mkuu, Mwenyekiti, mjumbe wa Bodi au mwajiriwa yeyote wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kufika mbele ya mchunguzi kwa ajili ya mahojiano na kujibu maswali.

(2) Mchunguzi anaweza kutoa nakala au kuchukua baadhi ya maelezo kutoka katika nyaraka zilizowasilishwa.

Ripoti ya uchunguzi.

50.-(1) Mchunguzi atawasilisha katika Ofisi ripoti ya uchunguzi ambayo imejumuisha taarifa yakinifu, matokeo na mapendekezo.

(2) Baada ya kupokea ripoti ya uchunguzi, Ofisi itaiwasilisha ripoti hiyo kwa Waziri anayehusika kwa mazingatio.

(3) Ofisi inaweza, endapo Waziri anayehusika hajachukua hatua yoyote kuhusiana na mapendekezo ya ripoti ya uchunguzi, kuwasilisha ripoti ya uchunguzi kwa Baraza la Mapinduzi.

SEHEMU YA SABA
KUUNDA UPYA KWA TAASISI ZA UWEKEZAJI ZA UMMA

Kuunda upya kwa Taasisi za Uwekezaji za Umma.

51.-(1) Endapo aina, malengo na maslahi ya kiuchumi ya Taasisi ya Uekezaji ya Umma yamebadilika au yamebadilika zaidi, Ofisi inaweza kuianisha Taasisi ya Uwekezaji ya Umma izingatiwe kwa kuunda upya.

(2) Baada ya kuanisha kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Ofisi itamtaarifu Waziri anayehusika.

Pendekezo la kuunda upya.

52.-(1) Msajili wa Hazina ataandaa na kuwasilisha kwa Waziri anayehusika pendekezo la kuunda upya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

(2) Pendekezo la kuunda upya lililoainishwa chini ya kifungu cha (1) cha kifungu hiki litajumuisha njia zilizopendekezwa za kuunda upya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

(3) Endapo Waziri anayehusika ameridhika na pendekezo la kuunda upya, Ofisi itawasilisha ripoti hiyo kwa Baraza la Mapinduzi kwa muongozo.

Hatua za dharura.

53.-(1) Endapo muongozo uliotoka Baraza la Mapinduzi unaelekeza kuunda upya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma, Ofisi inaweza, kwa tangazo lililochapishwa katika Gazeti, kutangaza kwamba utendaji wa Taasisi hiyo ya Uwekezaji ya Umma utakuwa chini ya usimamizi wa Ofisi.

(2) Ofisi inaweza kuteua uongozi wa mpito kutekeleza utendaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Tangazo la kuvunja.

54. Ofisi itaanzisha utaratibu wa kufunga Taasisi ya Uwekezaji ya Umma endapo pendekezo la kuvunja limeidhinishwa na Baraza la Mapinduzi.

Uteuzi wa mfilisi.

55.-(1) Ofisi itateua mfilisi kwa madhumuni ya kufunga Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

(2) Mfilisi aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atatekeleza majukumu yake kama yalivyoelezwa katika hati ya uteuzi.

(3) Mfilisi anaweza kuhamisha mali yote au sehemu ya mali ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma kuwa katika dhamana kwa kipindi kilichoanishwa cha majukumu yake.

(4) Ofisi itaanzisha taratibu za ufilisi chini ya kifungu hiki.

Kuvunja Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

56. Taasisi ya Uwekezaji ya Umma inaweza kuvunjwa au kufungwa kwa amri iliyotolewa na Rais na kuchapishwa katika Gazeti.

SEHEMU YA NANE
USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA

Usimamizi wa mali za umma.

57.-(1) Ofisi itakuwa na majukumu yafuatayo kuhusiana na usimamizi wa mali za umma:

(a) kuandaa na kupitia sera za usimamizi wa mali za umma, miongozo, taratibu na maelekezo mbalimbali kwa ajili ya ufanisi wa usimamizi wa mali za umma;

(b) kulihifadhi Daftari la Mali kwa mali zote za Umma kuwa chini ya uhifadhi wa Serikali;

(c) kuidhinisha uimarishaji wa Daftari la Mali ili kuhakikisha linafuata sera, sheria, kanuni na taratibu;

(d) kufanya ukaguzi na tathmini ya mali katika Taasisi za Umma;

(e) kuhakikisha kwamba muundo unaohusiana na mali za umma unawekwa kwa mujibu wa viwango vinavyokubalika;

(f) kuhakikisha mali za umma zinaondoshwa kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na taratibu;

(g) kukusanya mali zilizoharibika kutoka katika Taasisi za Umma ili zifutwe na Serikali; na

(h) kuanzisha mfumo sahihi wa usimamizi wa mali za umma ndani ya Taasisi za Umma;

Majukumu ya Afisa Masuuli.

58. Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuhakikisha kwamba mali za umma zilizo chini ya usimamizi wake zinahifadhiwa ipasavyo na kurekodiwas kwa mujibu wa viwango vilivyopo;

(b) kuhakikisha mifumo ya udhibiti wa ndani kwa ajili ya utaratibu wa uhifadhi na matengenezo ya mali za umma inawekwa;

(c) kuhifadhi na kuimarisha kila muda Daftari la Mali za Umma kwa kujumuisha mali mpya za umma zinazopatikana na kuondosha vifaa vilivyoondolewa;

(d) kuhakikisha utaratibu wa kuhifadhi unawekwa ili kuondosha wizi, hasara, kupotea na matumizi mabaya;

(e) kuwa mhifadhi mkuu wa mali zote za umma chini ya Taasisi ya Umma husika; na

(f) kuhakikisha mali za umma zilizoharibika, zilizoathirika na zilizopata mabadiliko ya hadhi zinatolewa taarifa katika Ofisi kwa hatua zaidi.

Kuanzisha Kitengo cha Usimamizi wa Mali.

59.-(1) Kutakuwa na Kitengo cha Usimamizi wa Mali katika kila Taasisi ya Umma.

(2) Kitengo kilichoainishwa kwenye kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kitapatiwa watendaji wa kutosha.

(3) Kitengo cha Usimamizi wa Mali kitakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuimarisha Daftari la Mali za Umma lililo chini ya uhifadhi wake kwa kuzingatia uhaulishaji wa mali za umma;

(b) kuhakikisha kwamba mali zote za umma zilizo chini ya usimamizi wake zinahifadhiwa kwa usahihi; na

(c) kitawajibika na kitahusika kwa mali zote za Taasisi ya Umma husika.

Mfumo wa Usimamizi wa Mali.

60.-(1) Ofisi itaanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Mali utakaotumiwa na Taasisi za Umma.

(2) Kitengo cha Usimamizi wa Mali kitatumia Mfumo kwa ajili ya kusimamia mali zote za Taasisi za Umma.

(3) Ofisi itatoa miongozo kwa Taasisi za Umma kwa ajili ya matumizi bora na uendeshaji wa Mfumo.

Matumizi ya mali za umma.

61.-(1) Afisa Masuuli ataidhinisha matumizi ya mali za umma katika Taasisi yake husika.

(2) Afisa Masuuli atahakikisha kwamba mali za umma zinatumika kwa tija na manufaa kulingana na jukumu litakalotekelezwa.

(3) Mali za umma hazitatumika kwa ajili ya maslahi binafsi isipokuwa kama imeidhinishwa na Afisa Masuuli.

Kupatikana kwa mali za umma.

62. Taasisi ya Umma inaweza kupata mali kupitia ununuzi, ujenzi, uhaulishaji, utaifishaji, urithi, msaada au kwa njia nyengine yoyote inayofaa.

Kutaifisha mali.

63.-(1) Endapo Serikali itapata mali zozote kwa njia ya kutaifisha kutokana na amri ya Mahkama au maamuzi, mali hizo zitawasilishwa kwa Msajili wa Hazina kwa ajili ya uhifadhi.

(2) Msajili wa Hazina baada ya kupokea mali iliyotaifishwa atazisajili mali hizo katika Daftari la Mali za Umma.

(3) Msajili wa Hazina atakuwa na uwezo wa kugawa au kuondoa mali zilizotaifishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma.

Umiliki, usajili na uwekaji wa alama.

64.-(1) Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali.

(2) Ofisi itatoa miongozo ya usajili wa umiliki na uwekaji wa alama kwa mali za umma.

Uchakavu.

65. Ofisi itaanda miongozo ya aina za mali, njia za uchakavu na viwango kwa Taasisi za Umma.

Mpango wa Matengenezo ya Mali.

66.-(1) Kutakuwa na Mpango wa Matengenezo ya Mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa.

(2) Kitengo cha Usimamizi wa Mali kitatoa taarifa kwa maandishi kwa Afisa Masuuli kuhusiana na hali ya utekelezaji wa Mpango wa Matengenezo wa Mwaka.

(3) Taasisi ya Umma itatenga fedha katika bajeti yake kwa ajili ya utekelezaji bora wa Mpango wa Matengenezo wa Mwaka.

Uthamini.

67.-(1) Taasisi ya Umma itafanya uthamini au itawezesha kufanyika kwa uthamini wa mali za umma chini ya usimamizi wake kwa mujibu wa matakwa ya viwango vya uthamini vinavyokubalika.

(2) Taarifa za uthamini wa mali za umma zitaweka msingi wa kumbukumbu katika Daftari la Mali za Umma.

Uhaulishaji wa mali za umma.

68. Mali za umma hazitohaulishwa kutoka katika Taasisi moja ya Umma kwenda Taasisi nyengine ya Umma bila ya idhini ya Ofisi.

Uondoaji wa mali za umma.

69.-(1) Kutakuwa na Mpango wa Uondoaji wa Mali wa Mwaka utakaoandaliwa na kila Taasisi ya Umma na kuwasilishwa katika Ofisi.

(2) Taasisi ya Umma itaomba ruhusa kutoka katika Ofisi kwa ajili ya kuondoa mali za umma.

(3) Ofisi, kabla ya kutoa ruhusa kwa Taasisi ya Umma kuondoa mali za umma, itafanya ukaguzi.

(4) Baada ya kukamilisha utaratibu wa kuondoaji, Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma husika ataliimarisha Daftari la Mali za Umma ipasavyo.

(5) Taasisi ya Umma, isiyokuwa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma, itawasilisha mapato yanayotokana na uondoaji wa mali katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

(6) Mali zitaondolewa katika mwaka wa fedha husika wa Taasisi ya Umma kwa mujibu wa Mpango wa Uondoaji wa Mwaka.

(7) Ofisi itatoa miongozo kuhusu utaratibu wa uondoaji wa mali.

Kufuta mali za umma zilizoharibika.

70. Ofisi itatoa miongozo ya taratibu za kufuta mali za umma zilizoharibika.

Ukaguzi wa mali za umma.

71.-(1) Taasisi ya Umma itafanya ukaguzi wa mali za umma angalau mara moja kwa kila mwaka wa fedha au wakati mwengine pale itakapohitajika katika kutambua idadi, thamani, uwepo, na hali ya matumizi.

(2) Msajili wa Hazina atatoa miongozo kuhusu utaratibu unaohusiana na ukaguzi wa mali za umma.

Ubadilishaji wa mali za umma.

72.-(1) Kitengo cha Usimamizi wa Mali kitaandaa Mpango wa Ubadilishaji wa Mali wa Mwaka na kitawasilisha kwa Afisa Masuuli kwa ajili ya kuingizwa katika Mpango wa Manunuzi wa mwaka.

(2) Ofisi itatoa miongozo kuhusu utaratibu unaohusiana na ubadilishaji wa mali za umma.

SEHEMU YA TISA
MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Ofisi.

73. Fedha na rasilimali nyengine za Ofisi zitajumuisha:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya Ofisi;

(b) mikopo au misaada inayopokelewa na Ofisi kwa ajili ya kazi zake; na

(c) fedha nyengine zozote zinazoweza kupatikana kihalali katika Ofisi.

Bajeti.

74.-(1) Ofisi, si chini ya miezi miwili kabla ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, itaanda na itawasilisha kwa Waziri bajeti ya mwaka kwa ajili ya kuidhinishwa inayoonesha makadirio ya mapato yake na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Kwa madhumuni ya masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Ofisi inaweza, wakati wowote kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha, kuandaa na kuwasilisha kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa makadirio yoyote ya bajeti ya ziada kwa bajeti ya mwaka wa fedha wa sasa.

Hesabu na ukaguzi.

75.-(1) Ofisi itaweka hesabu na kumbukumbu za miamala yote na itahakikisha kwamba fedha zote zilizopokelewa au kulipwa na Ofisi zimehisabiwa ipasavyo.

(2) Taarifa za fedha za mwaka za Ofisi zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Taarifa ya Mwaka.

76.-(1) Ofisi, ndani ya miezi saba baada ya mwisho wa mwaka wa fedha, itaandaa au itawezesha kuandaliwa na itawasilisha kwa Waziri Taarifa za Mwaka.

(2) Taarifa ya Mwaka chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa taarifa yakinifu inayozingatia kazi za Ofisi katika mwaka huo wa fedha ambao unahusika, na itajumuisha:

(a) nakala ya taarifa za hesabu zilizokaguliwa za Ofisi pamoja na taarifa ya mkaguzi;

(b) taarifa ya utekelezaji ya Ofisi ya mwaka huo wa fedha; na

(c) taarifa nyengine muhimu za Ofisi kama zinavyohitajika na Sheria hii.

(3) Kwa upatikanaji wa taarifa kwa umma, baada ya idhini ya Waziri, taarifa ya mwaka ya Ofisi itachapishwa.

SEHEMU YA KUMI
MASHARTI MENGINEYO

Uteuzi wa Taasisi ya Umma.

77. Waziri, baada ya idhini ya Baraza la Mapinduzi, atateua Taasisi yoyote ya Umma kuwa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Majukumu ya Waziri.

78. Waziri ataidhinisha mpango mkakati, bajeti na waraka mwengine wowote unaohusiana na uendeshaji wa Ofisi.

Masharti ya mpito.

79. Mtu ambaye mara kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii amekuwa Mwenyekiti au mjumbe wa Bodi wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma atachukuliwa kuwa ameteuliwa kwa mujibu ya masharti ya Sheria hii kwa kipindi kilichobakia cha utumishi wake kama ilivyoamualiwa au chini ya Sheria husika iliyoianzisha, waraka ulioanzisha au Katiba ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma, na kutokana na masharti yanayomuhusu kama mjumbe mara baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

Kanuni.

80. Waziri anaweza kutunga Kanuni za jumla kwa ajili ya utekelezaji bora wa madhumuni yaliyoainishwa chini ya masharti ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya mwaka 2002.

81.-(1) Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya mwaka 2002 inafutwa.

(2) Bila kujali kufutwa kwa Sheria ya Mitaji ya Umma Nam.4 ya mwaka 2002, jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria iliyotajwa ambalo bado linatekelezwa wakati wa kuanza kutumika kwa Sheria hii litachukuliwa kuwa limetekelezwa chini ya masharti ya Sheria hii.

MADHUMUNI NA SABABU

Lengo kuu la Mswada huu ni kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Taasisi za Uwekezaji za Umma na kusimamia mali za umma. Mswada unaopendekezwa pia una lengo la kuimarisha maadili ya utawala bora katika Taasisi za Uwekezaji za Umma.

Mswada unaelezea uwezo wa Ofisi katika kuchunguza utekelzaji wa Taasisi za Uwekezaji za Umma na kuwaita Wenyeviti, wajumbe binafsi wa Bodi na Maafisa Watendaji Wakuu endapo Ofisi inaona inafaa. Mswada umeweka masharti kwa Msajili wa Hazina ya kuingia katika mkataba wa utendaji na Wenyeviti, wajumbe wa Bodi na Maafisa Watendaji Wakuu.

Mswada umegawanyika katika Sehemu Kuu Kumi:

Sehemu ya Kwanza inaelezea masharti ya awali ambayo yanajumuisha jina fupi na kuanza kutumika, matumizi na ufafanuzi wa maneno mbalimbali yaliyotumika katika Mswada huu.

Sehemu ya Pili inapendekeza masharti yanayohusiana na kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina. Sehemu hii inajumuisha masharti ya kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina, muhuri na nembo ya Ofisi, kazi na uwezo wa Ofisi. Sehemu hii pia inaelezea kuhusiana na uteuzi wa Msajili wa Hazina, kazi za Msajili wa Hazina, uwezo wa kukasimu majukumu, watendaji wa Ofisi na katazo kwa Msajili wa Hazina na Watendaji.

Sehemu ya Tatu inaweka masharti yanayohusika na kuanzisha kwa Taasisi za Uwekezaji za Umma. Sehemu hii inaelezea kwa kina juu ya masharti yanayohusiana na utaratibu wa kuanzisha Taasisi za Uwekezaji za Umma, uwasilishaji wa mapendekezo ya mradi, hadhi ya kisheria ya Taasisi za Uwekezaji za Umma. Sehemu hii pia inahusika na masharti ya uteuzi wa Afisa Mtendaji Mkuu, ajira za watendaji, masharti ya utumishi kwa watendaji, muundo wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma, Bodi ya Wakurugenzi, Katibu wa Bodi, muda wa Bodi, ukomo wa kuwa mjumbe, kuvunjwa kwa Bodi, majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi, Kamati za Bodi, Mikutano ya Bodi, kueleza maslahi ya mjumbe, maslahi ya Bodi na Mkutano Mkuu wa Mwaka.

Sehemu ya Nne inaweka masharti ya Uwajibikaji wa Taasisi za Uwekezaji za Umma. Sehemu hii inaelezea juu ya mpango mkakati, mkataba wa utendaji wa Afisa Mtendaji Mkuu, tathmini ya mkataba wa utendaji na mikataba ya Utendaji kwa wajumbe wa Bodi. Sehemu hii pia inaelezea kuhusu masharti ya utayarishaji wa mpango wa fedha, uwezo wa kukopa, uwezo wa kuwekeza, utayarishaji wa taarifa za fedha, matawi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma, kuwasilisha malipo kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali, na fedha na rasilimali za Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Sehemu ya Tano inahusika na masharti ya kuwasilisha taarifa katika Ofisi. Sehemu hii inajumuisha masharti yanayohusika na wajibu wa kuwasilisha taarifa na utaratibu kwa kuwasilisha taarifa.

Sehemu ya Sita imeeleza kwa kina masharti kuhusu ukaguzi na uchunguzi ambayo yakijumuisha uteuzi wa wakaguzi, uwezo wa kukagua, uwezo wa mchunguzi na taarifa ya uchunguzi.

Sehemu ya Saba inapendekeza masharti yanayohusiana na kuunda upya kwa Taasisi za Uwekezaji za Umma.Sehemu hii inaeleza masharti ya pendekezo la kuunda upya, hatua za dharura juu ya usimamizi wa mpito juu ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma, tangazo la kuvunja, uteuzi wa mfilisi na kuvunja Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Sehemu ya Nane imeelezea masharti kuhusu Usimamizi wa mali za umma na inatoa majukumu ya Afisa Masuuli, kuanzisha Kitengo cha Usimamizi wa Mali. Sehemu hii pia inaelezea masharti kuhusu Mfumo wa Usimamizi wa Mali, matumizi ya mali za umma, kupatikana kwa mali za umma, umiliki, usajili na uwekaji wa alama, uchakavu na uthamini. Sehemu hii pia inaelezea masharti ambayo yanajumuisha masharti ya kutaifisha mali, uhaulishaji wa mali za umma, ukarabati na uondoaji wa mali za umma.

Sehemu ya Tisa inaweka masharti ya Fedha ambayo yanajumuisha fedha za Ofisi, bajeti, hesabu na ukaguzi, na Taarifa ya Mwaka.

Sehemu ya Kumi inaelezea Masharti Mengineyo ambayo yanajumuisha majukumu ya Waziri, masharti ya mpito, kanuni, kufuta na kubakiza Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya mwaka 2002.

ZANZIBAR
14 Aprili, 2021

DKT. MWINYI TALIB HAJI
MWANASHERIA MKUU
ZANZIBAR

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI - ZANZIBAR 2018